# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)

### HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA

SHULE YA SEKONDARI KINYENCHE,
S. L. P 130,
**SHIRATI – RORYA.**

**SIMU:** 0782 280 799 Mkuu wa Shule
0621 880 032 Makamu Mkuu wa Shule
0784 656 148 Mtaaluma

BARUA PEPE: kinyenchesecschool@gmail.com

**JINA LA MWANAFUNZI.......................................................................................**

**FOMU YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA – 2024**

Uongozi wa Shule ya Sekondari **Kinyenche** unayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa mwaka 2024 katika shule ya sekondari **KINYENCH**E, kama mwanafunzi wa kutwa. Hongera sana kupata nafasi hii adimu.

**MAHALI ILIPO:-**

Shule ya Sekondari KINYENCHE ipo Mkoa wa Mara, Wilaya ya Rorya, Kata ya Kinyenche. Shule ipo umbali wa kilomita moja (1KM) kutoka barabara kuu ya Bukama – Busulwa.

**MUDA WA KUFUNGUA SHULE**

Shule itafunguliwa tarehe 08/01/2024 saa 7:00 Asubuhi. Tafadhali fika na vitu vyote vinavyohitajika ili uweze kusajiliwa. Zoezi la kupokelewa na kusajiliwa litafanyika kwa **siku 14** tangu shule kufunguliwa, **tafadhali zingatia muda ili kuepuka usumbufu utakaojitokeza baadae.**

**MAHITAJI MUHIMU YA KUJA NAYO SHULENI**.

1. Sare ya shule.
2. Begi la kubebea madaftari (Rangi nyeusi).
3. Mkebe wa vifaa vya Hisabati ( Oxford).
4. Madaftari 10 counter books ( Quire 3 au 4)
5. Kamusi (Dictionary) English to Kiswahili/ Kiswahili to English.
6. Kalamu ya wino(bluu/nyeusi), penseli na rula.
7. T-Shirt Rangi ya “dark blue” ya kola yenye nembo ya shule
8. Tracksuit rangi ya kijani Kwa ajili ya michezo.
9. Rimu paper moja A4.

**MAELEZO YA SARE YA SHULE.**

**WAVULANA:-**

- Shati mbili nyeupe mikono mifupi isiyobana.
- Suruali ya rangi ya Ugoro na Orange yenye upana wa sentimita 17 chini na marinda mawili kila upande.
- Soksi za rangi nyeusi.
- Viatu vyeusi visivyo na kisigino vya kufunga na Kamba.
- Nywele fupi na sio kipara.
- Sweta la rangi ya Blue
- Tai rangi ya Ugoro na Orange.

**WASICHANA:-**

- Shati mbili nyeupe mikono mifupi isiyobana.
- Sketi ya rangi ya Ugoro na Orange yenye rinda box katikati ( ndefu)
- Soksi ndefu za rangi nyeupe (STOCKING).
- Viatu vyeusi visivyo na kisigino vya kufunga na Kamba.
- Nywele fupi na sio kipara.
- Sweta la rangi ya Blue
- Skafu rangi ya Ugoro na Orange.

**SHERIA ZA SHULE**

**A. NIDHAMU KWA UJUMLA**

***Nidhamu kwa ujumla.***

1. Ni lazima mwanafunzi awahi shuleni asubuhi saa 12:30 na kufanya usafi wa mazingira ya shule na kuhudhuria gwaride la ukaguzi wa usafi na kuchangamsha mwili.
2. mwanafunzi yeyote haruhusiwi kuondoka katika eneo la shule bila kupata kibali kutoka kwa mwalimu wa darasa, mwalimu wa zamu au idara ya malezi.
3. Mwanafunzi anatakiwa kusimama, kusalimia na kuwapokea mzigo walimu au mtu yeyote mwenye umri mkubwa zaidi yake popote akutanapo na watu wa aina hiyo.
4. Haruhusiwi kutumia **LUGHA CHAFU** miongoni mwa wanafunzi na kwa mtu mwingine yeyote.
5. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wanafunzi wenzake, viranja na wafanyakazi wote shuleni.
6. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya darasani na shughuli za michezo na uzalishaji mali kulingana na ratiba.
7. Mwanafunzi lazima afanye mitihani ya masomo yote anayosoma shuleni hapa.
8. Mwanafunzi awapo shuleni hairuhusiwi kuwa na aina yeyote au vitu vifuatavyo:-
   Kucha ndefu, Kupaka rangi, kuvaa cheni na herein, nywele ndefu, kunyoa kipara, kunyoa nyusi, kupaka dawa nywele n.k.
9. Mwanafunzi ahakikishe kuwa awapo mahali popote ndani na nje ya shule awe amevaa nguo za heshima. Ni marufuku kuvaa nguo zinazobana, fupi na nyepesi.

10. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo zaidi ya zile zilizotajwa katika maelezo ya kujiunga na shule, ikiwemo sweta la ranga inayotakiwa.
11. Wanafunzi wanatakiwa kutunza mali zao binafsi na mali za shule. Pia wanatakiwa kutoa taarifa kwa utawala juu ya uharibifu wa mali za shule.
12. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kwenda kwenye maeneno yafuatayo bila sababu maalumu au bila kupewa ruhusa.
    a) Shule za jirani.
    b) Nyumba zinazozunguka shule.
    c) Vibanda vya Biashara nje ya shule.
13. Ni marufuku mwanafunzi kukutwa sehemu zifuatazo:-
    a) Baa, Klabu za usiku, Vibanda vya kuonyesha mipira n.k.
    b) Nyumba za kulala wageni isipokuwa akiwa na wazazi au walezi wake.
14. Wawapo shuleni wanafunzi hawaruhusiwi kumiliki vitu vya gharama kama; Simu ya mkononi, redio, kamera, ipad, albam za picha na CD.
15. Kila mwanafunzi ni lazima afanye bidi katika kila somo.
16. Hakikisha ukimya wa hali ya juu unazingatiwa katika maeneo yote ya shule na ya kujifunzia hasa darasani, Maktaba, Maabara na kwenye korido wakati wa vipindi.
17. Adhabu ya viboko itaruhusiwa kwa kosa linalostahili na kuwa na taarifa/ kibali cha mkuu wa shule.
18. Hakikisha muda wote unapokuwa shuleni unaongea lugha ya Kiingereza nje na ndani ya darasa.
19. Mwanafunzi Yeyote akikamatwa na kitu Chochote kisichotakiwa shuleni mfano ( rejea namba 14) kitaharibiwa mbele ya yake/ mbele ya wanafunzi wenzake.
20. Mwanafunzi akiharibu mali ya shule kama vile madawati, Meza, fensi n.k. atagharamia matengenezo.

**B. MAKOSA AMBAYO MWANAFUNZI AKIFANYA ANAWEZA KUFUKUZWA SHULE.**

1. Kutokuchukua ripoti ya maendeleo yake ya nusu mwaka au mwaka.
2. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
3. Aina zote za wizi na unyang'anyi.
4. Aina zote za makossa ya kujamiana na uasherati. Hii ni pamoja na mikanda ya video, vitabu vichafu vya uasherati au vitu vinavyofanana na hivo.
5. kupiga au kupigana.
6. Matumizi ya lughachafuyamatusi.
7. Makosa ya jinai.
8. Kuzomea watumishi au kuchokoza wanafunzi wengine.
9. Kugoma au kuchochea mgomo (ghasia).
10. Kutohudhuia shuleni kwa muda wa siku 30 bila taarifa atasimamishwa masomo, siku 90 mfululizo bila taarifa atafukuzwa shule.
11. KudharauBenderayaTaifa.
12. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule, (Pia ikithibitika kutoa mimba).
13. Kuoa au kuolewa.
14. Kukuwadia mwanafunzi mwenzake na mtumishi yeyote katika mambo ya mapenzi ndani nan je ya shule.
15. Kunyanyasa mwanafunzi mwenzake kutokana na jinsia yake, udini, ulemavu, ugeni wake au hali yake.

16. Kughushi mitihani au wizi wa mtihani, kukataa au kutofanya mitihani na mazoezi ya masomo bila sababu za msingi.
17. Kukataa adhabu kwa makusudi. Pia adhabu inaweza kutolewa na mwalimu au kiranja yeyote kwa mwanafunzi anayeonesha utovu wa nidhamu.
18. kuharibu mali ya Shule kwa makusudiikiwa ni pamoja na majengo, mali ya mtu au kundi la watu.
19. Kukamatwa na simu, Redio, kamera, ipad, albam za picha na CD kwa mara ya pili baada ya kuonywa kwa mara ya kwanza.
20. Uvutaji wa sigara na bangi.
21. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

**C. WAJIBU WA MZAZI.**

1. Mzazi/Mlezi anatakiwa kumleta mwanae kumwandikisha shuleni anapoanza masomo.
2. Mzazi/Mlezi anatakiwa kuandikisha majina ya watu wanne na namba zao za simu watakaohurusiwa kupata ripoti za mtoto akiwa shuleni na mawasialino ya vikao, wito n.k.
3. Mzazi/Mlezi anatakiwa kuja kuchukuwa ripoti ya mtoto wake kwa muhula husika vinginevyo hatapokelewa muhula unaofuata.
4. Mzazi/ Mlezi anatakiwa kufika shuleni kwa muda muafaka pindi anapohitajika na uongozi wa shule.
5. Mzazi/ Mlezi ajenge tabia ya kutembelea shule mara kwa mara ili kujua maendeleo ya mtoto wake badala ya kusubiri kuitwa ili kujenga mshikamano wa malezi.
6. Mzazi/ Mlezi amfahamu kwa jina na namba ya simu Mwalimu wa darasa la mtoto wake ili kujenga mahusiano ya malezi ya mtoto.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU**.

**OBADIA MANG'ERA**

**MKUU WA SHULE.**

**MUHIMU:**

**Fomu zilizoambatanishwa zinatakiwa zijazwe kikamilifu na zirudishwe shuleni**.

1. Fomu rasmi ya kuandikishwa.
2. Ahadi ya Mwanafunzi na Mzazi/Mlezi
3. Fomu ya uchunguzi wa Daktari.

**KINYENCHE SECONDARY SCHOOL.**
**P.O. BOX 130**
**SHIRATI – RORYA.**

A RECOGNISED MEDICAL DOCTOR MUST FILL THIS FORM.

To the Medical Officer.

.................................................. Hospital
..................................................

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

Please examine........................................................ (Name of Student) who has been selected to join this school for his/her fitness as a student in the following areas:-

1. Eye sight.........................................................................
2. Hearing...........................................................................
3. Specimens:-
   a) Urine.........................................................................
   b) Blood........................................................................
   c) Stool.........................................................................
4. Asthma...........................................................................
5. Tuberculosis.....................................................................
6. Pregnancy (for girls)..............................................................
7. Diabetes...........................................................................
8. HIV.................................................................................
9. Hepatitis.........................................................................
10. Others..........................................................................................................................
    ...........................................................................................................................

**MEDICAL CERTIFICATE**
(To be completed by Medical Doctor)
I..................................................................................... (Name of the Medical Doctor)

Have examined the above and considered that he/she is fit/ not fit to be enrolled as a student.

Signature.............................................................................

Designation..........................................................................

Official Stamp.....................................................................

Date.....................................................................................

**KIAMBATISHO "A"**

**FOMU RASMI YA KUANDIKISHWA.**

Sehemu hii ijazwe na mwanafunzi.

1. Jina kamili la mwanafunzi........................................................................
2. Uraia..................................................................................................
3. Dini....................................................................................................
4. Tarehe ya kuzaliwa.................................................................................
5. Mahali ulipozaliwa..................................................................................
6. Yatima/ Sio yatima/ Mzazi mmoja (kata isiyohusika)
7. Shule uliyosoma kabla ya kuja sekondari.......................... (jaza jedwali)

| JINA LILILOANDIKISHWA SHULENI | SHULE YA MSINGI ULIYOTOKA | MWAKA ULIOANZA | MWAKA ULIOMALIZA |
|---|---|---|---|
| | | | |

Saini ya Mwanafunzi........................................................... Tarehe...................................

Sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi........................................................................

1. Jina kamili la Mzazi / Mlezi...................................................................
2. Uraia...............................................................................
3. Anuani kamili ya Sehemu unayoishi................................... Wilaya..........................
4. Mtaa......................................................
5. Kata..............................................
6. Namba za simu........................................................................... (ya haraka).

**Melezo ya Kikazi ya Mzazi/Mlezi.................................................................**

1. Jina la Mwajiri na Idara.........................................................................
2. Anuani..................................................................................................
3. Namba za simu.......................................................................................
4. Kazi ya Mzazi/Mlezi.............................................................................
   (Karani, Meneja, Mkulima, Mfanyabiashara n.k.)
5. Saini ya Mzazi/Mlezi...................................................... Tarehe.....................

**KIAMBATANISHO "B"**

## AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi.........................................................................................................

1. Nimeyasoma na kuyaelewa maelezo yote na nimekubali kujiunga na shule hii ya sekondari **KINYENCHE** kuanzia leo tarehe..........................................................

2. **Naahidi kwamba:**
   a) Nitazingatia sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa.
   b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakua kinyume na Serikali ya Jumhuri ya Muungano wa Tanzania.
   c) Nitatunza mali za Umma ambayo ni pamoja na Majengo, Samani, Vitabu na Vifaa vya Maabara.
   d) Nipo tayari kuchukuliwa hatua yoyote stahiki endapo nitakiuka maelezo yaliyotolewa kwenye fomu hii.

## AHADI YA MZAZI/MLEZI

**Mimi Mzazi/Mlezi wa........................................................................ Kidato cha....................**

**Naahidi kwamba:-**

a) Nitashirikiana kikamilifu na Uongozi wa Shule na walimu wote kwa ujumla katika kumuelimisha na kumlea mtoto wangu. Hii ni kuhakikisha kuwa atatii sheria zote za shule na kuyazingatia mambo yote muhimu yaliyotajwa.
b) Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu kufika shuleni kila siku kabla ya saa 1:00 asubuhi.
c) Na kwamba mwanafunzi atahitimu na kufuzu kidato cha kwanza hadi cha nne.
d) Ninaruhusu mwanangu achukuliwe hatua yoyote stahiki endapo atavunja mojawapo ya sheria na kanuni zilizo orodheshwa.

**Saini ya Mzazi/Mlezi............................................................ Tarehe...............................**